**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

**MHESHIMIWA IDRISSA KITWANA MUSTAFA**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**IMEWASILISHWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2026**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Subhaanahu Wa Ta'ala, kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa, kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako likae kwa madhumuni ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2025/2026 na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

3. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Viongozi wetu Wakuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wao madhubuti unaoendelea kuleta maendeleo na kudumisha amani na utulivu nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kipekee nitumie fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mweyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kunipa imani na kuendelea kuniamini kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Baraza hili na kuniteua tena kushika dhamana ya Uwaziri wa Ofisi yake hii. Ninaahidi kuitumikia dhamana hii kwa uadilifu na uwajibikaji kwa maslahi mapana ya wananchi wetu na taifa letu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, namshukuru Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla; Makamu wa Pili wa Rais kwa

ushauri na maelekezo yake yenye mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu.Kwa hakika usimamizi wake kwetu unatupa ari na kujiamini zaidi katika kufanya kazi zetu.

6. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani maalum ziende kwa Waziri alienitangulia kwenye ofisi hii ambae ni Mheshimiwa Masoud Ali Mohammed Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa uongozi wake ulioacha dira na misingi imara katika kuendeleza ofisi hii. Ofisi inathamini jitihada zake za kujenga mshikamano, kuimarisha utendaji na kusimamia vyema utekelazaji wa miradi mikubwa ya kimkakati. Ofisi itaendelea kutekeleza vyema dira na maono aliyoyaweka ili kuleta matokeo zaidi kwa manufaa ya taifa.

7. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti na Katibu wa Baraza kwa uongozi na ushirikiano wenu katika kuendesha shughuli za Baraza hili Tukufu. Ofisi yangu itaendelea kutoa ushirikiano kwa uongozi wa Baraza lako kila itapohitajika.

8. **Mheshimiwa Spika,** Kadhalika, naishukuru kwa dhati Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu ya Baraza lako Tukufu, ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Aza Januari Joseph kwa ushauri na ufuatiliaji wao katika kusimamia utendaji wa Ofisi yetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ambao ni Mheshimiwa Mahmoud Shineni Ali, Mheshimiwa Zaina Abdalla Salum, Mheshimiwa Mmanga Mohammed Hemed, Mheshimiwa Masoud Amour Masoud, na Mheshimiwa Mahfoudh Abdalla Mohammed kwa mchango wao mkubwa katika kuimarisha majukumu ya Ofisi.

10. **Mheshimiwa Spika,** Kwa umuhimu wake, napenda kutambua na kuwashukuru Makatibu wa Kamati kwa kuratibu kwa ufanisi shughuli za Kamati na kuimarisha mawasiliano pamoja na ushirikiano kati ya Kamati na Ofisi yangu.

11. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi na shukurani hizo, sasa naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka 2025/2026, pamoja na Mwelekeo wa Ofisi kwa mwaka 2026/2027.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA UJUMLA

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi kwa ujumla iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **427,910,104,000/=.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **208,985,900,000/=** ni mishahara, Shilingi **48,469,777,000/=** ni matumizi mengineyo, Shilingi **20,436,300,000/=** ni ruzuku na Shilingi **150,018,127,000/=** ni kazi za maendeleo.

13. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, Ofisi ilipokea na kutumia jumla ya Shilingi **224,488,296,895/=** sawa na asilimia **52** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **143,215,252,524/=** sawa na asilimia 68 ni mishahara, Shilingi **30,738,920,157/=** sawa na asilimia 63 ni matumizi mengineyo, Shilingi **12,135,820,460/=** sawa na asilimia **59** ni ruzuku na Shilingi **38,398,303,755/=** sawa na asilimia **25** ni kazi za maendeleo. **(Kiambatanisho namba 01 kinafafanua zaidi**)

**TATHMINI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA KUCHANGIA MFUKO MKUU WA HAZINA**

14. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi iliidhinishiwa kukusanya Shilingi **10,858,070,000/=** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya Shilingi **4,349,311,993/=** zimekusanywa sawa na asilimia **40** ya makadirio ya mwaka. **(Kiambatanisho namba 02 kinafafanua).**

15. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji huu upo chini ya matarajio kutokana na changamoto mbali mbali, ikiwemo kuchelewa kulipwa kwa madeni ya Wakala wa Ulinzi JKU, mwamko mdogo wa wananchi katika kusajili matukio yao ya kijamii kwa wakati pamoja na wananchi kutohaulisha umiliki wa ardhi.

**TATHMINI YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA SERIKALI ZA MITAA**

16. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lako Tukufu liliidhinisha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato ya Shilingi 1**9,169,264,087/=** kwa ujumla. Hadi kufikia Machi 2026, Mamlaka hizo zimefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **12,695,246,310/=** sawa na asilimia **66** ya makadirio ya mwaka. (Kiambatanisho namba 03 kinafafanua zaidi).

**TATHMINI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KILA FUNGU**

17. **Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa kuwasilisha utekelezaji wa bajeti ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kila programu zinazosimamiwa na kutekelezwa na Ofisi kama ifuatavyo:-

**MAKAO MAKUU YA WIZARA – FUNGU D01**

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Idara za Makao Makuu ziliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi **100,616,970,000/=.** Hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizopatikana kwa matumizi ni shillingi **23,159,082,175/=** sawa na asilimia **23** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,739,577,469/=** sawa na asilimia **76** zimetumika kulipa mishahara, Shilingi **2,626,671,570/=** sawa na asilimia 44 ni matumizi mengineyo (OC) na Shilingi **18,690,923,469/=** sawa na asilimia **20** ni kazi za maendeleo.

19. **Mheshimiwa Spika,** Fungu la Makao Makuu ya Wizara lilidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **1,800,000,000/=,** hadi kufikia Machi, 2026 imekusanya Shilingi **1,999,917,000,000/=** sawa na asilimia **111** ya makadirio ya mwaka.

**JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) – FUNGU D02**

20. **Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Kujenga Uchumi liliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **71,852,300,000/=**, hadi kufikia Machi, 2026, limeingiziwa Shilingi **50,065,077,556/=** sawa na asilimia 69 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **33,629,879,307/=** sawa na asilimia **71** zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **6,650,072,761/=** sawa na asilimia **67** ni matumizi mengineyo, Shilingi **204,575,000/=** sawa na asilimia **27** ni Ruzuku ya Wakala wa Ulinzi wa JKU na Shilingi **9,580,550,488/=** sawa na asilimia **65** ni kazi za maendeleo.

21. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Jeshi la Kujenga Uchumi liliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **3,079,418,000/=** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina, hadi kufikia Machi 2026, limekusanya shilingi **670,869,342.44/=** sawa na asilimia 22 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha

hizo, JKU Makao Makuu ilipangiwa kukusanya shilingi **379,418,000/=** na kukusanya shilingi **166,000,000/=** sawa na asilimia 44, na Wakala wa Ulinzi JKU ulipangiwa kukusanya Shilingi **2,700,000,000/=** na kukusanya shilingi **504,869,342.44/=** sawa na asilimia **19** ya makadirio ya mwaka.

**CHUO CHA MAFUNZO – FUNGU D03**

**22. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Mafunzo kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **41,992,700,000/=,** hadi kufikia Machi, 2026, kilipatiwa matumizi ya Shilingi **29,267,658,446/=** sawa na asilimia **69** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **23,090,062,442/=** sawa na asilimia **72** zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **4,562,596,004/=** sawa na asilimia **68** ni matumizi mengineyo na Shilingi **1,615,000,000/=** sawa na asilimia **45** ni kazi za maendeleo.

**23. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Chuo cha Mafunzo kiliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **297,089,000/=** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina na kufanikiwa kukusanya Shilingi **180,700,000/=** sawa na asilimia **61** ya makadirio ya mwaka.

**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO – FUNGU D04**

**24. Mheshimiwa Spika,** Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **69,655,300,000/=,** hadi kufikia Machi, 2026, kilipatiwa matumizi ya Shilingi **40,727,860,025/=** sawa na asilimia **58** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **33,194,015,577/=** sawa na asilimia **60** zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **6,037,688,633/=** sawa na asilimia **63** ni matumizi mengineyo na Shilingi **1,496,155,815/=** sawa na asilimia **29** ni kazi za maendeleo.

**25. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **290,760,000/=** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina na

kufanikiwa kukusanya Shilingi **50,000,000/=** sawa na asilimia **17** ya makadirio ya mwaka.

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI – FUNGU D05**

**26.Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **54,538,957,000/=,** hadi kufikia Machi 2026, Kikosi kiliingiziwa matumizi ya Shilingi **25,674,627,929/=** sawa na asilimia 47 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1**8,207,446,701/=** sawa na asilimia **72** zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **3,197,020,536/=** sawa na asilimia **83** ni matumizi mengineyo na Shilingi **4,270,160,692/=** sawa na asilimia **16** ni kazi za maendeleo.

**27. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **458,138,000/=** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina na kufanikiwa kukusanya Shilingi **132,061,000/=** sawa na asilimia **29** ya makadirio ya mwaka.

**KIKOSI CHA VALANTIA – FUNGU D06**

**28. Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) kiliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **44,864,900,000/=,** hadi kufikia Machi 2026, Kikosi kiliingiziwa Shilingi **28,855,988,301/=** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **23,965,668,364/=** sawa na asilimia 68 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **3,704,303,638/=** sawa na asilimia 85 ni matumizi mengineyo na Shilingi **1,186,016,299/=** sawa na asilimia **21** ni kazi za maendeleo.

**MKOA WA MJINI MAGHARIBI – FUNGU D07**

**29. Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Mjini Magharibi uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **13,500,600,000/=,** hadi kufikia Machi

2026, Mkoa uliingiziwa Shilingi **8,205,359,492.50/=** sawa na asilimia **61** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,869,356,472.50/=** sawa na asilimia **72** zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **716,379,037/=** sawa na asilimia **37** ni matumizi mengineyo na Shilingi **5,619,623,983/=** sawa na asilimia 6**3** ni Ruzuku kwa Mabaraza ya Manispaa na Baraza la Jiji.

**30.Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mkoa wa Mjini Magharibi uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **80,504,000/=** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina, hadi kufikia Machi, 2026 Mkoa umekusanya mapato ya Shilingi **24,890,000/=** sawa na asilimia **31** ya makadirio ya mwaka.

**31. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa ya Mjini liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **3,880,000,000/=,** hadi kufikia Machi, 2026, Baraza limekusanya Shilingi **2,309,167,482/=** sawa na asilimia **60** ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Baraza la Manispaa Magharibi 'A' liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **2,530,000,000/=,** na kufanikiwa kusanya Shilingi **1,863,237,418/=** sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Baraza la Manispaa Magharibi 'B' liliidhinishiwa kukusanya Shilingi **2,901,674,000/=** na kufanikiwa kukusanya Shilingi **1,802,980,901/=** sawa na asilimia **62** ya makadirio ya mwaka.

**MKOA WA KUSINI UNGUJA – FUNGU D08**

**32. Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kusini Unguja, uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **4,710,577,000/=.** Hadi kufikia Machi, 2026 Mkoa ulipokea na kutumia Shilingi **3,493,982,140.5/=** sawa na asilimia **74** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,435,657,330/=** sawa na asilimia 76 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **732,612,800/=** sawa na asilimia 73 ni matumizi mengineyo, Shilingi **1,280,038,011/=** sawa

na asilimia 71 ni Ruzuku ya Baraza la Manispaa Kati na Baraza la Mji Kusini na Shilingi **45,674,000/=** sawa na asilimia **49.6** ni fedha za Washirika wa Maendeleo.

**33. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mkoa wa Kusini Unguja uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **58,561,000/=** kwa lengo la kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia Machi, 2026, Mkoa umekusanya Shilingi **12,526,001/=** sawa na asilimia **21** ya makadirio ya mwaka.

**34. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Kati liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani Shilingi **1,955,000,000/=** na kufanikiwa kukusanya Shilingi **1,061,107,761/=** sawa na asilimia 54 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Baraza la Mji Kusini liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **1,243,740,000/=** na kufanikiwa kukusanya Shilingi **1,156,198,670/=** sawa na asilimia **93** ya makadirio ya mwaka.

**MKOA WA KASKAZINI UNGUJA – FUNGU D09**

**35. Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kaskazini Unguja uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **5,614,500,000/=**. Hadi kufikia Machi 2026, Mkoa ulipokea na kutumia Shilingi **3,432,939,791/=** sawa na asilimia **61** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,516,414,135/=** sawa na asilimia 72 zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **426,000,000/=** sawa na asilimia **43** matumizi mengineyo, Shilingi **1,444,061,731/=** sawa na asilimia **57** ni ruzuku ya Manispaa ya Kaskazini ‘A’ na Baraza la Mji Kaskazini ‘B’ na Shilingi **46,463,925/=** sawa na asilimia **61** ni fedha za Washirika wa maendeleo.

**36. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mkoa wa Kaskazini Unguja uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **35,000,000/=** kwa lengo la kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia Machi 2026, Mkoa umekusanya Shilingi **4,250,000/=** sawa na asilimia **12** ya makadirio ya mwaka.

37. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Kaskazini 'A' liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **2,841,922,087/=.** Hadi kufikia Machi 2026, Manispaa ya Kaskazini 'A' imefanikiwa kukusanya Shilingi **1,871,764,477/=** sawa na asilimia **66** ya makadirio ya mwaka. Aidha, Baraza la Mji Kaskazini 'B' liliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **1,534,500,000/=** na kufanikiwa kukusanya Shilingi **878,797,852/=** sawa na asilimia **57** ya makadirio ya mwaka.

**MKOA WA KUSINI PEMBA – FUNGU D10**

38. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **6,218,900,000/=.** Hadi kufikia Machi 2026, Mkoa ulipokea na kutumia Shilingi **3,798,629,779.5/=** sawa na asilimia **62** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,106,285,052.50/=** sawa na asilimia **68** zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **548,166,000/=** sawa na asilimia **54** ni matumizi mengineyo, Shilingi **2,085,112,727/=** sawa na asilimia **59** ni ruzuku ya Baraza la Manispaa Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani na Shilingi **59,066,000/=** sawa na asilimia **64** ni fedha za Washirika wa maendeleo.

39. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **40,596,000/=** kwa lengo la kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia Machi 2026, Mkoa ulikusanya mapato ya Shilingi **18,226,000/=** sawa na asilimia **44** ya makadirio ya mwaka.

40. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Chake chake liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **880,788,000/=** na kufanikiwa kukusanya Shilingi **621,795,075/=** sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Baraza la Mji Mkoani liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **426,640,000/=** na kufanikiwa kuvuka lengo kwa kukusanya Shilingi **464,932,437/=** sawa na asilimia **109** ya makadirio ya mwaka.

## MKOA WA KASKAZINI PEMBA – FUNGU D11

41. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kaskazini Pemba uliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **5,464,500,000/=**. Hadi kufikia Machi 2026, Mkoa ulipokea na kutumia Shilingi **3,227,017,188.50/=** sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,225,475,847.50/=** sawa na asilimia **75** zilitumika kulipa mishahara, Shilingi **540,000,000/=** sawa na asilimia **43** ni matumizi mengineyo, Shilingi **1,400,499,341/=** sawa na asilimia **54** ni ruzuku ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na Shilingi **61,042,000/=** sawa na asilimia **66** ni fedha za Washirika wa maendeleo.

42. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Mkoa ulipangiwa kukusanya mapato ya Shilingi **20,000,000/=** kwa lengo la kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia Machi 2026, Mkoa ulikusanya mapato ya Shilingi **1,011,000/=** sawa na asilimia **5** ya makadirio ya mwaka.

43. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Wete liliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **505,000,000/=** na kufanikiwa kukusanya Shilingi **325,710,925/=** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya mwaka. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni iliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani ya Shilingi **470,000,000/=** na kufanikiwa kukusanya Shilingi **339,553,312/=** sawa na asilimia **72** ya makadirio ya mwaka.

## WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII – FUNGU D12

44. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi **8,934,200,000/=.** Hadi kufikia Machi 2026, Wakala ulipokea na kutumia Shilingi **4,580,074,071/=** sawa na asilimia **51** ya makadirio

ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,235,413,826/=** sawa na asilimia **70** zilitumika kwa kulipa mishahara, Shilingi **997,409,178/=** sawa na asilimia **44** ni matumizi mengineyo na Shilingi **1,347,251,067/=** sawa na asilimia **38** ni kazi za maendeleo.

45. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii uliidhinishiwa kukusanya mapato ya Shilingi **4,698,004,000/=** kwa lengo la kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia Machi 2026, Wakala umekusanya Shilingi **1,254,861,650/=** sawa na asilimia **27** ya makadirio ya mwaka.

## C. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA PROGRAMU KWA MWAKA 2025/2026

### MALENGO YALIYOTEKELEZWA NA MAKAO MAKUU YA OFISI

46. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi kupitia Idara za Makao Makuu imefanikiwa kutekeleza malengo mbali mbali kama ifuatavyo:-

### Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Shehia 48

47. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Ofisi za Shehia 48, ambapo 28 zipo Unguja na 20 Pemba. Ujenzi wa Ofisi hizo upo katika hatua mbali mbali za umaliziaji, ambapo kukamilika kwake kutawezesha Masheha kuhudumia wananchi katika Ofisi rasmi za umma na kuboresha utoaji wa huduma za Serikali katika ngazi ya Shehia. **(Kiambatanisho nambari 04 kinafafanua maeneo ya ujenzi)**

**Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya**

48. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imekamilisha maandalizi muhimu ya michoro, makisio ya gharama na upatikanaji wa maeneo ya ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa. Kwa upande wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya maandalizi yake bado yanaendelea katika hatua mbali mbali. Mradi huu unalenga kuboresha mazingira ya kazi na kutatua changamoto ya ufinyu na uchakavu wa ofisi zilizopo. (Kiambatanisho nambari 05 kinafafanua maeneo ya ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa)

**Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi Ngazi za Jamii (SCALE)**

49. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeanza kutekeleza Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Ngazi ya Jamii, chini ya ufadhili wa mkopo wa Benki ya Dunia. Katika hatua za awali za utekelezaji, Ofisi imeandaa miongozo mitatu, ambayo ni Mwongozo wa uibuaji wa fursa na vikwazo kwa wananchi, Mwongozo wa kupokea na kutatua malalamiko ya wananchi pamoja na Mwongozo wa mawasiliano kati ya wananchi na mradi. Lengo la miongozo hii ni kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu na kunufaika na utekelezaji wa mradi huu.

**Mradi wa Kijani Pemba (GREEN AND SMART CITY - SASA)**

50. **Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa mradi wa Kijani Pemba unaofadhiliwa na msaada wa Umoja wa Ulaya, Ofisi imeendelea kusimamia ukarabati mdogo wa viwanja viwili vya mpira Micheweni pamoja na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha kukuza na kuwalea wajasiriamali wadogo Michakaeni. Aidha, Mradi unaendelea kuwawezesha vijana 300 kutoka Wilaya zote za Pemba kupata mafunzo ya ujuzi kupitia vyuo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali vya Daya Mtambwe na Vitongoji, hatua inayowawezesha vijana hao kujiajiri na kupata kipato.

**Mradi wa Haki Jinai - Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Hanyegwa Mchana**

51. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi inaendelea kutekeleza mradi wa Haki Jinai ambao unahusisha ujenzi wa Chuo cha Mafunzo kipya cha kisasa katika eneo la Hanyegwa Mchana. Mradi huu utakapokamilika, utawezesha kuhamishwa kwa Chuo cha Mafunzo Kiinua Miguu kwenda katika majengo mapya ya kisasa na salama. Hivyo, mradi huu utaboresha mazingira ya Chuo cha Mafunzo na kuongeza ufanisi wa utoaji wa mafunzo ya urekebishaji tabia kwa wanafunzi na mahabusu katika viwango vinavyokubalika kimataifa.

**Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar**

52. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar kwa kufunga miundombinu ya ulinzi ya kisasa katika maeneo ya Kimkakati. Utekelezaji wa Mradi huu umeongeza ufanisi wa Idara Maalum za SMZ katika kutekeleza majukumu yao ya kiulinzi na kuimarisha hali ya usalama kwa manufaa ya nchi na wananchi wake.

**Kuimarisha Utumishi wa Idara Maalum za SMZ**

53. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha masuala ya kiutumishi ndani ya Idara Maalum za SMZ, Tume imefanikiwa kuandaa na kutoa miongozo miwili muhimu inayohusu nyongeza ya muda wa utumishi na upandishaji wa vyeo. Aidha, Tume imefanya vikao vinne vilivyojadili na kutoa suluhisho la changamoto mbali mbali za kiutumishi, hatua hizo zimesaidia kupunguza malalamiko ya watumishi wa Idara Maalum za SMZ.

**Kuunda Mabaraza ya Madiwani nchini**

**54. Mheshimiwa Spika,** Kufuatia kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, Ofisi imetekeleza kikamilifu takwa la kisheria la kuunda Mabaraza ya Madiwani nchini. Jumla ya Mabaraza 12 yameanzishwa na kutangazwa rasmi kupitia Tangazo la Kisheria namba 146 la mwaka 2025. Hatua hii imeimarisha Utawala Bora na ushiriki wa wananchi katika maamuzi ya maendeleo ngazi ya chini. **(Kiambatanisho namba 06 kinafafanua)**

**Maendeleo ya NGO's Nchini**

**55. Mheshimiwa Spika,** Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGO's) zimeendelea kuwa wadau muhimu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo nchini, ambapo kupitia uratibu wa Kisera na Kisheria, zimeelekezwa kuendana na vipaombele vya Kitaifa na kuchangia ustawi wa wananchi. Katika kipindi cha miezi tisa iliyopita, Ofisi imesajili Jumuiya 20 na kufikisha Jumuiya zilizosajiliwa Zanzibar kuwa 1,069. Mchango wa Jumuiya hizo umeonekana zaidi katika sekta za afya, elimu, ustawi wa jamii na mazingira.

**Maendeleo ya Viwanda vya Idara Maalum za SMZ**

**56. Mheshimiwa Spika,** Ofisi imepata mafanikio katika kuviendeleza viwanda vya Idara Maalum za SMZ, vinavyotoa huduma muhimu za kiushoni, ikiwemo nguo, mikoba, viatu na machapisho mbali mbali. Viwanda vilipatiwa mashine mpya za kisasa za uzalishaji ambazo zimeongeza tija na ubora wa bidhaa tunazozizalisha.

## MALENGO YALIYOTEKELEZWA NA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D02-D06)

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara Maalum za SMZ imesimamia na kutekeleza yafuatayo;

**Kutoa mafunzo ya malezi ya Vijana (JKU)**

58. **Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Kujenga Uchumi (Fungu D02) limeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuwalea na kuwaendeleza vijana kwa kuwapatia mafunzo ya ukakamavu, uzalendo na kazi za amali, sambamba na kutoa mafunzo ya ufundi na elimu ya sekondari. Jeshi la Kujenga Uchumi limefanikiwa kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana 1,238, mafunzo ya kilimo, ufugaji, uvuvi pamoja na uzalendo kwa vijana 4,146 na mafunzo ya elimu ya Sekondari kwa Vijana 1,344 kupitia Skuli ya JKU Mtoni.

59. **Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Kujenga Uchumi limeendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa kuendelea na ujenzi wa Nyumba za Watumishi Ng'ambwa Pemba ambapo Ujenzi umefikia asilimia 70, Ujenzi wa Dakhalia ya Skuli ya Sekondari ya JKU umefikia asilimia 40, Ujenzi wa Makao Makuu JKU Saateni umefikia asilimia 15 pamoja na ujenzi wa Ofisi za Wakala wa Ulinzi wa JKU ambao umefikia asilimia **60.**

**Kutoa huduma za urekebishaji tabia Chuo Cha Mafunzo**

60. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Mafunzo kimeweza kutoa huduma za urekebishaji tabia kwa Wanafunzi na Mahabusu wake. Chuo cha Mafunzo kilipokea jumla ya wanafunzi na mahabusu 748 ikilinganishwa na kipindi cha mwaka 2024/2025 ambapo kilipokea jumla ya wanafunzi na mahabusu 722. Takwimu hii inatupa tafsiri ya kutoengezeka kwa kasi ya uhalifu nchini kutokana na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwekeza katika kuwaletea wananchi wake maendeleo.

61. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi ya maendeleo, Chuo cha Mafunzo kimekamilisha ujenzi wa Hanga katika kambi ya Bumbwini na kuendelea na Ujenzi wa Nyumba tisa za maafisa na wapiganaji katika kambi ya Hanyegwa Mchana ambapo ujenzi wake umefikia asilimia **80.**

**Ulinzi na Uokozi Baharini**

62. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanikisha shughuli zake za ulinzi na usalama baharini kupitia doria za ulinzi baharini zilizofanyika. Matukio mbali mbali ya uvunjaji wa sheria baharini yaliweza kudhibitiwa na shughuli za uokozi baharini zimeweza kutekelezwa. Kikosi kimefanikiwa kukamata matukio 46 ya biashara ya magendo. Aidha, katika shughuli za uokozi, Kikosi kimewaokoa wananchi 141 ambapo 122 wakiwa hai na wananchi 19 wakiwa wameshafariki.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi ya maendeleo kikosi kimefanya manunuzi ya vifaa vya uokoaji baharini vyenye thamani ya Shilingi **1,297,443,519.98/=** ambazo tayari zimelipwa na vifaa vimekabidhiwa KMKM.

**Kutoa huduma za zimamoto na uokozi**

64. **Mheshimiwa Spika,** Katika miradi ya maendeleo, Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga uwezo wa Kikosi chetu cha Zimamoto kwa kukipatia gari mpya za kisasa 19, boti ya kisasa ya zimamoto, pampu kubwa sita na seti 53 za vifaa vya uokozi baharini. Kadhalika, Kikosi kimewezeshwa kujenga vituo vitatu vya zimamoto katika eneo la Bwejuu, Kibuteni na Chamanangwe sambamba na kuwezeshwa kujenga hanga katika Kambi ya Mkanyageni Pemba.

65. **Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa shughuli mahsusi, Kikosi cha KZU kimeweza kutoa huduma za zimamoto na

uokozi katika matukio 473 yaliyoripotiwa Unguja na Pemba. Matukio hayo yamepelekea wananchi 24 kupoteza maisha na kufanikiwa kuokoa maisha ya wananchi 43. Aidha, Kikosi kimetoa huduma zake kwenye viwanja vya ndege na bandari, huduma ambazo zimesaidia kuonesha kimataifa usalama wa viwanja vyetu vya ndege na Bandari zetu.

**Kufanya Operesheni na doria za ulinzi**

66. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao, Kikosi cha Valantia Zanzibar kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya Ulinzi na Usalama SMZ na SMT kimeendelea kufanya Operesheni na doria za ulinzi kote nchini. Kikosi hiki kimekuwa kikifanya doria za mara kwa mara katika maeneo ya ndani ya miji na vijiji, ambapo kwa wastani doria hufanyika mara tatu hadi nne kwa wiki.

67. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Valantia kupitia Kitengo chake cha QRF (Quick Reaction Force) kinachukua hatua za haraka kwa kufika kwa wakati katika maeneo yote yanayotambuliwa kuwa hatarishi ili kuimarisha ulinzi na kuzuia uhalifu kabla haujatokea au kuenea.

68. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Valantia kimekamilisha mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya KVZ Muyuni na kuendeleza ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Makao Makuu ya KVZ Mtoni na hospitali ya KVZ Ndugukitu Pemba ambapo ujenzi wa hospitali hizo umefikia asilimia 65. Aidha, Kikosi kimeendelea na ujenzi wa mahanga 15 katika Kambi za KVZ Pangatupu, Kiashangwe, Micheweni na Pujini ambapo ujenzi wa mahanga hayo umefikia wastani wa asilimia **75.**

**Wakala wa Ulinzi JKU**

69. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ulinzi JKU unaendelea kuimarisha utoaji na usimamizi wa huduma za kiulinzi kwa lengo la kuhakikisha maeneo ya uwekezaji husus an sekta ya utalii yanakuwa salama. Wakala wa Ulinzi umefanikiwa kutoa huduma za ulinzi kwa Makampuni 40, taasisi binafsi 117 na taasisi za Serikali 98. Aidha, Wakala wa Ulinzi umefanikiwa kufanya doria 584 katika maeneo ya uwekezaji na biashara Unguja na Pemba.

70. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ulinzi JKU kwa sasa imeanzisha kitengo cha usajili wa Kampuni za Ulinzi ili kuakisi takwa la kisheria kwa mujibu wa Sheria namba 2 ya mwaka 2015 Sheria ya Wakala wa Ulinzi JKU ambapo moja ya majukumu yake ni kutoa miongozo ya kiulinzi kwa niaba ya Serikali.

**Kutoa huduma za Afya kwa Maafisa, Askari na Wananchi**

71. **Mheshimiwa Spika,** Idara Maalum za SMZ zimeendelea kuimarisha huduma za Afya katika Kambi zake kwa lengo la kuhakikisha Maafisa, Wapiganaji na Wananchi wanapata huduma za Afya zilizokua bora. Jumla ya Wagonjwa wa nje (OPD) 204,630 walipatiwa huduma za Afya katika Hospitali na Vituo vya Afya vinavyomilikiwa na Idara Maalum za SMZ. Aidha, Idara Maalum za SMZ zimefanikiwa kuwapeleka masomoni wahudumu wa afya 98 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutoa huduma za afya kwa ufanisi.

**Kuchochea Sekta ya michezo na utamaduni nchini**

72. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuchochea sekta ya michezo na utamaduni, Vikosi vya Idara Maalum vya SMZ vinaendelea kuibua na kukuza vipaji vya wanamichezo pamoja na kuimarisha ushiriki wao katika mashindano mbali mbali yanayoandaliwa ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa mafanikio ya kujivunia ni kuona timu za vikosi vyote vya

SMZ vinashiriki katika mashindano ya ligi kuu za Zanzibar ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa wavu na mpira wa pete.

73. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa utamaduni, Vikundi vya sanaa vya vikosi vyetu vimekuwa mstari wa mbele kushiriki na kutoa burudani katika matamasha na hafla mbali mbali za kitaifa, ikiwemo maadhimisho ya miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na uzinduzi wa miradi ya maendeleo.

**Ujenzi wa barabara za ndani zinazoenda Makambini**

74. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, imesimamia ujenzi wa barabara zinazoelekea katika makambi ya Idara Maalum za SMZ Unguja na Pemba. Miongoni mwa Kambi zilizonufaika na ujenzi wa barabara hizo za lami ni pamoja na Kambi ya Chuo cha Mafunzo Hanyegwa Mchana na Kambi ya KMKM Kama.

**MALENGO YALIYOTEKELEZWA NA MIKOA (FUNGU D07-D11)**

75. **Mheshimiwa Spika,** Upande wa Tawala za Mikoa unajumuisha Mikoa mitano, Wilaya 11, Wilaya ndogo mbili (2) na Shehia 388, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 umefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria nambari 08 ya mwaka 2014 kama ifuatavyo:-

**Kusimamia Usalama, Amani na Utulivu Ndani ya Mikoa**

76. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Nchi yetu ilifanya Uchaguzi Mkuu ambao ulimalizika bila ya kuathiri amani na utulivu tulionao. Nichukue nafasi hii kuzipongeza Ofisi za Mikoa na Wilaya, Vyombo vya ulinzi na Usalama, Vyama vyetu vya siasa na Wananchi kwa ujumla kwa mashirikiano mazuri waliyoyatoa kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu ambayo kiukweli mashirikiano hayo yamesaidia kuhakikisha nchi yetu inabaki salama, amani na utulivu.

**77. Mheshimiwa Spika,** Jitihada kubwa zimeendelea kuchukuliwa na Ofisi za Mikoa, Wilaya na Shehia kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama kwa nia ya kulinda, kuenzi na kutunza amani, utulivu na mshikamano wa wananchi katika maeneo yetu mbali mbali. Jumla ya Doria na Operesheni maalum 348 zilifanyika na mikutano maalum 106 ya kuhubiri na kuwasisitiza wananchi kutunza amani imefanyika.

**Usuluhishi wa migogoro ya ardhi**

**78. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza takwa la kisheria, Ofisi za Mikoa, Wilaya na Shehia zimeendelea kusuluhisha migogoro mbali mbali inayojitokeza katika maeneo yao. Jumla ya migogoro 187 ya ardhi iliripotiwa, ambapo migogoro 76 imetatuliwa na 111 inaendelea kufanyiwa kazi. Utatuzi wa migogoro ngazi ya Mkoa na Wilaya umesaidia wananchi wetu kupata haki zao kwa wakati. **(Kiambatanisho namba 07 kinafafanua)**

**Kuratibu Mpango wa Kupambana na Udhalilishaji**

**79. Mheshimiwa Spika,** Ofisi za Mikoa na Wilaya zimeendelea kuratibu na kusimamia Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto. Katika kipindi kilichopita, jumla ya vikao 146 na mikutano Shirikishi ya wananchi 88 imefanyika. Hatua hii imewezesha Mikoa kuweka mikakati madhubuti katika kupinga vitendo hivyo, pamoja na kuongeza uelewa na ujasiri wa wananchi kuripoti matukio ya udhalilishaji yanayotokea katika maeneo yao.

**Kusimamia na Kufuatilia Miradi ya Maendeleo**

**80. Mheshimiwa Spika,** Mikoa imefanikiwa kutekeleza wajibu wake wa kisheria wa kusimamia na kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao. Katika kipindi husika, jumla ya miradi 116 ilifuatiliwa kupitia ziara na

vikao mbali mbali, ambapo miradi 47 imekamilika. Ufuatiliaji huu umeimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi na kuharakisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi. **(Kiambatanisho namba 08 kinafafanua zaidi)**

**Ukimbizaji wa Mwenge wa Uhuru Kitaifa**

81. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya zilifanikiwa kukamilisha maandalizi ya ukimbizaji wa Mwenge wa Uhuru katika maeneo yao, ambapo Mkoa wa Kusini Pemba ulikuwa mwenyeji wa sherehe za uzinduzi wake kitaifa. Mwenge huo umeangazia na kukagua miradi ya maendeleo katika kila Wilaya, hatua iliyochochea ushiriki wa wananchi katika kutambua miradi inayotekelezwa na Serikali yao.

**Ufuatiliaji wa Ahadi na Maagizo ya Viongozi Wakuu**

82. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi za Wakuu wa Mikoa zimeendelea kutekeleza jukumu lake la kufuatilia utekelezaji wa Ahadi na maagizo ya viongozi wakuu wa kitaifa katika maeneo yao, ambapo jumla ya ahadi 28 zilifuatiliwa na utekelezaji wake kufanywa na taasisi husika. Ufuatiliaji huu umeimarisha uwajibikaji wa taasisi za serikali na kuhakikisha wananchi wanapatiwa ufumbuzi wa changamoto zao kwa wakati.

**MALENGO YALIYOTEKELEZWA NA SERIKALI ZA MITAA**

83. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa hapa Zanzibar ni 12, ambazo zimegawika katika hadhi ya Jiji, Manispaa, Miji na Halmashauri. Mamlaka hizi zinafanya kazi zake chini ya Sheria nambari 7 ya mwaka 2014 pamoja na Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2012. Katika kipindi cha utekelezaji, mafanikio mbali mbali yamepatikana kama ifuatavyo:-

**Kuimarisha usafi wa Miji**

84. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango katika kuboresha huduma za usafi wa miji kwa kukabidhi kwa wakandarasi maeneo 111 ya ujenzi wa vituo vidogo vya kukusanyia taka, ambapo maeneo 73 yapo Unguja na 38 Pemba. Aidha, mkataba wa ununuzi na usambazaji wa magari 26 ya taka umeingiwa, ambapo magari hayo yanatarajiwa kuanza kupokelewa mwezi Juni 2026.

85. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanikiwa kuingia Mkataba na Kampuni binafsi ya uendeshaji wa Jaa la Kibele pamoja na kusimamia zoezi la kuondoa majaa yasiyo rasmi 52 katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kadhalika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kukusanya na kuondoa taka katika maeneo rasmi ya utupaji. Hatua hizi zilizochukuliwa zimeimarisha mfumo wa usimamizi wa taka katika maeneo yetu.

**Uwezeshaji wa Wajasiriamali kupitia Mikopo ya 4:4:2**

86. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya 4:4:2 inayotolewa kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Mamlaka zetu zimefanikiwa kutoa jumla ya shilingi **642,605,374.82** kuwasilisha katika Mfuko wa Makundi Maalum unaosimamiwa na Mamlaka ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumu (ZEEA). Mikopo hii imewezesha wajasiriamali wadogo kupata mitaji inayoinua kipato chao na kuwawezesha kuimarisha maisha yao ya kila siku. **(Kiambatanisho nambari 09 kinafanunua fedha zilizowasilishwa ZEEA).**

## MIRADI YA MAENDELEO YA SERIKALI ZA MITAA

87. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kutumia mapato yake ya ndani katika kutekeleza na kusimamia miradi mbali mbali ya maendeleo kama ifuatavyo:-

88. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Mjini kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), limefanikiwa kusimamia ujenzi wa Soko la Mombasa, ambalo limekamilika na sasa linaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

89. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Magharibi A limefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Stendi ya Daladala Mndo, ambayo inaendelea kutoa huduma kwa wananchi wetu. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa Stendi ya Daladala Mambosasa yamekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

90. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Kaskazini A limeendelea na ujenzi wa Soko la Chaani ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 60. Aidha, jitihada zinaendelea kuchukuliwa kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa manufaa ya wanachi wetu.

91. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Kaskazini 'B' limefanikiwa kukamilisha mradi wa ujenzi wa Soko la Kitope ambalo kwa sasa linaendelea kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, Baraza limeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa Soko la Mahonda ambalo ujenzi wake umefikia asilimia **30.**

92. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Kati limekamilisha ujenzi wa Bustani ya Jamii Hanywegwa Mchana pamoja na kukamilisha ujenzi wa vituo vinne vya kusubiria daladala. Aidha, Baraza limekamilisha maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha kuchakata taka Chwaka.

93. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa ya Chake Chake limefanikiwa kukamilisha kujenga uzio wa Bustani ya Mwanamashungi pamoja na kutangaza zabuni ya uendeshaji wa Bustani hiyo. Hatua hii inalifanya eneo hilo kuwa salama zaidi na lenye kutoa huduma bora kwa wananchi.

94. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Mkoani limefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Soko la Wananchi Kengeja na kuendelea na ujenzi wa soko la wananchi Kendwa Kiwani. Aidha, Baraza limekamilisha ujenzi wa vituo vinane vya kusubiria Daladala. Ujenzi wa masoko hayo umelenga kuwawekea mazingira salama wajasiriamali wa maeneo ya Kengeja na Kiwani.

95. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Wete limeendeleza ujenzi wa Soko la Mzambarauni ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 80 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2026. Aidha, Baraza limekamilisha maandalizi ya ujenzi wa Soko la Kojani pamoja na ujenzi wa Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Weni.

**MALENGO YALIYOTEKELEZWA NA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU -D12)**

96. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu lake la kisheria la kusajili matukio ya kijamii nchini, Wakala umefanikiwa kutekeleza yafuatayo :-

**Ujenzi wa Miundombinu ya Matukio ya Kijamii**

97. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanikiwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Mahonda Wilaya ya Kaskazini B, ambao umefikia asilimia **50.** Mradi huu unalenga kuondosha changamoto ya utoaji wa huduma za usajili wa matukio ya kijamii kwa wananchi wa Wilaya ya Kaskazini B.

98. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi inaendelea na mradi wa ujenzi wa Kituo cha urejeshaji wa huduma za usajili baada majanga ambapo ujenzi wake umefikia asilimia **50.** Kukamilika kwa mradi huu kutahakikisha kumbukumbu za usajili wa matukio ya kijamii hazipotei wakati wa majanga na huduma zinaendelea bila kusimama.

**Kuimarisha mifumo ya kidijitali**

99. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imepiga hatua katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa kuimarisha na kuendesha mifumo ya usajili wa kidijitali inayolenga kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Katika kipindi kilichopita, jumla ya mifumo minane ya Taasisi za Serikali imeunganishwa na mfumo mkuu wa usajili wa matukio ya kijami. Kadhalika, zoezi la kuhifadhi kumbukumbu za zamani kwa njia ya kidijitali limeendelea kutekelezwa.

**Uhamasishaji wa Usajili wa Matukio ya Kijamii**

100. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kufanya juhudi za makusudi kuhamasisha wananchi kusajili matukio yao ya kijamii kupitia vipindi vilivyoandaliwa na kurushwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijami. Jumla ya wananchi 6,046 walifikiwa na vipindi hivyo kupitia YouTube, Instagram na Facebook, hatua inayoonesha mwitikio mzuri wa wananchi kuhamasika.

**Matukio ya Kijamii Yaliyosajiliwa**

101. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imefanikiwa kusajili vizazi 47,292 vifo 2,381, ndoa 4,947 na talaka 490. Kadhalika, Ofisi imesajili na kutoa vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi 23,175. Usajili huu umeimarisha utambuzi wa wananchi na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma katika sekta mbali mbali.

## D. MWELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**102. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, mafungu ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yatasomeka kama ifuatavyo:-

1. Fungu 004 - Idara za Makao Makuu ya Wizara
2. Fungu 041 - Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii
3. Fungu 042- Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)
4. Fungu 043- Chuo cha Mafunzo
5. Fungu 044- Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)
6. Fungu 045- Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU)
7. Fungu 046- Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ)
8. Fungu 047 - Mkoa wa Mjini Magharibi
9. Fungu 048 - Mkoa wa Kaskazini Unguja
10. Fungu 049 - Mkoa wa Kusini Unguja
11. Fungu 050 - Mkoa wa Kusini Pemba
12. Fungu 051 - Mkoa wa Kaskazini Pemba

### MALENGO YA MIPANGO NA BAJETI YATAKAYOTEKELEZWA NA MAKAO MAKUU YA WIZARA (FUNGU 004)

**103. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Makao Makuu ya Wizara kupitia fungu 004 imepanga kutekeleza malengo ya mipango na bajeti kama ifuatavyo:-

### MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA

**104. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara zake itasimamia na kutekeleza Miradi ifuatayo:-

i. Kuanza Mradi wa ujenzi wa Chuo cha Kijeshi cha Idara Maalum za SMZ.

ii. Kuanza Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ.
iii. Kukamilisha Mradi wa ujenzi wa Chuo Kipya cha Mafunzo Hanyegwa Mchana.
iv. Kuendeleza Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar.
v. Kuanza mradi wa ujenzi wa soko la Kibandamaiti na soko la Kinyasini;
vi. Kuanza Mradi wa Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi katika Bwawa la Mwanakwerekwe;
vii. Kusimamia Mradi wa Usafi na Upendezeshaji wa Miji ambapo Serikali itaajiri Kampuni binafsi zenye uwezo wa kimataifa;
viii. Kusimamia na kutekeleza Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya tabia nchi ngazi ya jamii (SCALE)
ix. Kusimamia Mradi wa "Green and Smart City" SASA Pemba;
x. Kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Ofisi 276 za Shehia;
xi. Kusimamia Mradi wa Ujenzi wa Ofisi tano za Mikoa.

**SHUGHULI MAHSUSI ZITAKAZOSIMAMIWA NA WIZARA**

**105. Mheshimiwa Spika,** Mbali na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Wizara kupitia Idara zake imepanga kutekeleza shughuli mahsusi zifuatazo:-

i. Kufanya utafiti wa chanzo cha mapato ya leseni za biashara katika Manispaa za Unguja na Pemba;
ii. Kufanya tathmini ya uendeshaji wa masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi, Chuini na Mombasa;
iii. Kukamilisha Rasimu ya Sera ya Usimamizi wa Taka Ngumu Zanzibar;
iv. Kufanya maboresho ya kina ya mfumo wa pamoja wa ukusanyaji mapato ya Serikali za Mitaa (Zan - MUTM);
v. Kufasiri miongozo ya Serikali Kuu Kwenda Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
vi. Kuratibu uanzishwaji wa Kanzi data (Database) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vii. Kuweka mazingira wezeshi kwa NGO’s Zanzibar;
viii. Kusimamia upatikanaji wa stahiki za watumishi na vitendea kazi kwa wakati.

**MALENGO YATAYOTEKELEZWA NA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU 041)**

**106. Mheshimiwa Spika,** Ofisi kupitia Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kupitia fungu 041 imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusajili Watoto wote walio chini ya umri wa miaka mitano.
ii. Kusajili na kuingiza kumbukumbu za ndoa na talaka ndani ya mfumo wa kidijitali.
iii. Kuimarisha huduma za vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, Vitambulisho vya wafanyakazi na vitambulisho vya Wazanzibar waishio nje ya nchi (Diaspora).
iv. Kumalizia ujenzi wa Mradi wa Ofisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Mahonda na Mradi wa ujenzi wa Kituo cha urejeshaji huduma baada ya maafa.
v. Kuuboresha mfumo Mkuu wa usajili wa matukio ya kijamii.
vi. Kutoa huduma za Utawala na Uendeshaji.

**MALENGO YATAYOTEKELEZWA NA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU 042-046)**
**MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**

**107. Mheshimiwa Spika,** Miradi ya maendeleo ifuatayo itasimamiwa na kutekelezwa na Idara Maalum.

i. Kukamilisha Mradi wa ujenzi wa Hospitali za KVZ Mtoni na Ndugukitu.
ii. Ununuzi wa meli ya KMKM pamoja na kukamilisha mradi wa vituo vya uzamiaji na uokozi KMKM Kizimkazi na Ukunjwi.

iii. Kukamilisha mradi wa ujenzi wa Dakhalia ya Skuli ya Sekondari JKU Mtoni.
iv. Kukamilisha mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wakala wa Ulinzi JKU.
v. Kukamilisha mradi wa ujenzi wa Ofisi kuu ya KZU Chanjaani Pemba na
vi. Kukamilisha ujenzi wa majengo ya Chuo Cha Mafunzo Kinumoshi, Tungamaa, Ubago na Kengeja.

**SHUGHULI MAHSUSI ZITAKAZOTEKELEZWA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**

**108.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Idara Maalum za SMZ zimepanga kutekeleza shughuli mahsusi zifuatazo: -

**JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) – FUNGU 042.**

**109.** **Mheshimiwa Spika,** JKU imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
i. Kutoa mafunzo ya Uzalendo na uzalishaji mali kwa vijana.
ii. Kukuza uzalishaji wa chakula nchini.
iii. Kutoa huduma za ulinzi na usalama
iv. Kushiriki katika majanga na huduma za dharura.
v. Kuimarisha skuli ya ufundi na skuli ya sekondari JKU Mtoni.
vi. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala

**CHUO CHA MAFUNZO (MF) - FUNGU 043**

**110.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Mafunzo kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -
i. Kutoa huduma za urekebishaji kwa wanafunzi na mahabusu wa Chuo cha Mafunzo
ii. Kutoa mafunzo ya stadi za kazi na ujasiriamali kwa wanafunzi

iii. Kutunza na kukuza haki za binaadamu na ustawi wa wanafunzi
iv. Kuboresha shughuli za uzalishaji mali
v. Kutoa huduma za ulinzi na usalama.
vi. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala

**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - 044.**

**111. Mheshimiwa Spika,** Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa huduma za ulinzi na usalama baharini na nchi kavu.
ii. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji kwa wakati.
iii. Kuimarisha huduma za afya Hospitali ya KMKM Kibweni.
iv. Kushirikiana na Kampuni binafsi katika miradi ya kibiashara ya KMKM

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) – FUNGU 045**

**112. Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU) kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa huduma za zimamoto na uokozi Bandarini, Viwanja vya ndege na kwenye Manispaa.
ii. Kukamilisha rasimu za Sheria na Sera za Zimamoto na Uokozi.
iii. Kutoa huduma za ulinzi na usalama.
iv. Kutoa elimu ya usalama wa moto na uokozi.
v. Kufanya ukaguzi wa usalama wa moto kwenye Taasisi na vyombo vya usafiri.
vi. Kuendeleza mashirikiano na Washirika wa Maendeleo
vii. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala wa kikosi kwa ufanisi.

## KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) – FUNGU 046

113. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Valantia (KVZ) kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i.Kuimarisha ulinzi na doria.
ii.Kuimarisha huduma za utawala na uendeshaji
iii.Kuwajengea uwezo Maafisa na Wapiganaji
iv.Kuimarisha huduma za afya na
v.Kuendeleza huduma za utamaduni na michezo.

## MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA MIKOA (FUNGU 047-051)

114. **Mheshimiwa Spika,** Tawala za Mikoa kupitia fungu 047 hadi 051 zimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kusimamia usalama, amani na utulivu ili kuiwezesha Zanzibar kuendelea kuwa Kisiwa cha amani;
ii. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na shughuli za kisekta ndani ya Mikoa;
iii. Kushughulikia migogoro inayojitokeza ikiwemo migogoro ya ardhi ngazi ya Shehia, Wilaya na Mikoa;
iv. Kuratibu shughuli za kitaifa ikiwemo ukimbizaji wa Mwenge wa Uhuru kwa kila Wilaya;
v. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali SMZ na SMT;
vi. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mpango Mkuu wa kupambana na udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto;
vii. Kuandaa mikakati ya kupambana na wizi wa mazao na mifugo;
viii. Kuandaa na kukamilisha mipango mikakati ya maendeleo ya Mikoa;
ix. Kufanya vikao vya Kamati za Maendeleo za Mikoa;
x. Kuratibu upatikanaji wa misaada kwa wananchi wasiojiweza na wanaoishi katika mazingira magumu;
xi. Kushajihisha wananchi kutunza mazingira na afya zao;

xii. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala ngazi ya Mikoa, Wilaya na Shehia.

**MALENGO YATAYOTEKELEZWA NA SERIKALI ZA MITAA**

**115. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuhakikisha zinatoa huduma bora kwa wananchi wa maeneo yao zimepanga kutekeleza mipango ya Miradi ya Maendeleo ifuatayo:-

**MIRADI YA MAENDELEO ITAYOTEKELEZWA NA SERIKALI ZA MITAA**

i. Manispaa ya Mjini imepanga kujenga jengo la Biashara katika eneo la Kwa Hajitumbo.
ii. Manispaa ya Magharibi 'A' imepanga kujenga Stendi ya Daladala katika eneo la Mambosasa.
iii. Manispaa ya Magharibi 'B' imepanga kujenga maegesho katika eneo la soko la Mombasa pamoja na kuanza ujenzi wa Soko la Kisauni.
iv. Manispaa ya Kaskazini 'A' imepanga kukamilisha ujenzi wa Soko la Chaani Masingini na ujenzi wa kituo cha daladala Nungwi.
v. Baraza la Manispaa Kati limepanga kuanza ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia Watoto Tunguu.
vi. Manispaa ya Chake Chake imepanga kufanya ukarabati mkubwa wa Chinjio la Tibirinzi.
vii. Baraza la Mji Kaskazini 'B' limepanga kukamilisha ujenzi wa Soko la Mahonda.
viii. Baraza la Mji Wete limepanga kujenga Soko la Kojani na kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Weni.
ix. Baraza la Mji Mkoani limepanga kukamilisha ujenzi wa Soko la Kendwa Kiwani na kuanza ujenzi wa Soko la Michenzani.
x. Baraza la Mji Kusini limepanga kujenga stendi ya daladala Makunduchi na kuanza maandalizi ya ujenzi wa Soko la Kitogani.

xi. Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imepanga kujenga Soko la Micheweni.

**SHUGHULI MAHSUSI ZITAZOTEKELEZWA NA SERIKALI ZA MITAA**

**116. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea kutekeleza majukumu yake ya kimsingi kwa kutekeleza shughuli mahsusi zifuatazo: -

i. Kuweka mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato (Database);
ii. Kuweka mifumo bora ya ukusanyaji wa taka kutoka majumbani na maeneo ya biashara.
iii. Kuanzisha mashindano ya usafi kwa kila Shehia.
iv. Kufanya usafi wa mitaro ya maji ya mvua na maeneo ya wazi
v. Kufanya matengenezo ya miundombinu ikiwemo taa za barabarani, taa za kuongozea gari na alama za barabarani.
vi. Kuchangia fedha za mapato ya ndani asilimia 10 kwenda Mfuko Mkuu wa Uwezeshaji Makundi Maalum.
vii. Kufanikisha utekelezaji na shughuli mtambuka kama vile uhifadhi wa mazingira, Kampeni za kujikinga na maambukizi ya VVU na hifadhi ya mtoto.
viii. Kutoa misaada kwa wananchi wanaopatwa na maafa.
ix. Kusimamia na kuratibu vikao vya Kamati za mashauriano za Shehia na Mabaraza ya Wadi.
x. Kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Serikali za Mitaa.
xi. Kutoa elimu kwa wananchi juu ya majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.
xii. Kushiriki katika matamasha na Sherehe za kitaifa.
xiii. Kuweka mazingira wezeshi ya viwanja vya sikukuu.
xiv. Kuhakikisha upatikanaji wa vitendea kazi na malipo ya stahiki za Madiwani na watendaji.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

117. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuweza kutekeleza malengo yaliyokusudiwa, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ifuatavyo:-

## MAKAO MAKUU YA WIZARA (FUNGU 004)

118. **Mheshimiwa Spika,** Fungu 004 (Idara za Makao Makuu) linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 366,485,276,440/=. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,647,490,000/= ni mishahara, Shilingi 5,012,800,000/= ni matumizi mengineyo, Shilingi 792,480,000/= ni ruzuku ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ, Shilingi 358,032,506,000/= kwa kazi za maendeleo ambapo Shilingi 7,855,886,440/= ni fedha za Washirika wa Maendeleo. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 1,857,000,000/= yatakayokusanywa na kuchangiwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

## WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU 041)

119. **Mheshimiwa Spika,** Fungu 041 (Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii) linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **9,148,649,150/=** Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,993,250,000/=** ni mishahara, Shilingi **1,898,150,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **4,257,249,000/=** kwa kazi za maendeleo. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **3,253,999,000/=** yatakayokusanywa na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

## JESHI LA KUJENGA UCHUMI - FUNGU 042

120. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **70,805,770,000/=** kwa fungu 042 la Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU). Kati ya fedha hizo Shilingi **47,883,000,000/=** ni mishahara, Shilingi **9,336,800,000/=** ni matumizi mengineyo, Shilingi **822,690,000/=** ni ruzuku ya Wakala wa Ulinzi JKU na Shilingi **12,763,280,000/=** ni kazi za maendeleo.

121. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **2,325,000,000/=** yatakayokusanywa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo Shilingi **675,000,000/=** zitakusanywa na Jeshi la Kujenga Uchumi na Shilingi **1,650,000,000/=** zitakusanywa na Wakala wa Ulinzi wa JKU.

## CHUO CHA MAFUNZO - FUNGU 043

122. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **50,169,540,000/=** kwa fungu 043 la Chuo cha Mafunzo. Kati ya hizo, Shilingi **39,793,570,000/=** ni mishahara, Shilingi **6,975,970,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **3,400,000,000/=** ni kazi za maendeleo. Aidha, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **375,000,000/=** yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

## KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO - FUNGU 044

123. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **72,330,280,000/=** kwa fungu 044 la Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Kati ya fedha hizo, Shilingi **51,200,000,000/=** ni mishahara, Shilingi **8,346,280,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **12,784,000,000/=** ni kazi za maendeleo. Aidha, Fungu hili

linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **375,700,000/=** yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI - FUNGU 045**

124. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **38,692,331,000/=** kwa fungu 045 la Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU). Kati ya fedha hizo, Shillingi **26,239,930,000/=** ni mishahara, Shillingi **4,893,410,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **7,558,991,000/=** ni kazi za maendeleo. Vile vile, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **467,500,000/=** yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR – FUNGU 046**

125. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **47,622,760,000/=** kwa fungu 046 la Kikosi cha Valantia (KVZ). Kati ya fedha hizo Shillingi **36,746,750,000/=** ni mishahara, Shillingi 4**,476,010,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **6,400,000,000/=** ni kazi za maendeleo.

**MKOA WA MJINI MAGHARIBI (FUNGU 047)**

126. **Mheshimiwa Spika,** Fungu 047 (Mkoa wa Mjini Magharibi) linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **14,170,930,000/=.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,647,470,000/=** ni mishahara, Shilingi **2,420,440,000/** ni matumizi mengineyo na Shilingi **9,103,020,000/=** ni ruzuku kwa Baraza Jiji la Zanzibar, Baraza la Manispaa Mjini, Baraza la Manispaa Magharibi A na Baraza la Manispaa Magharibi B. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **42,392,000/=** yatakayokusanywa na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**127. Mheshimiwa Spika,** Ofisi inaomba kuidhinishiwa mapato ya shilingi **4,975,893,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Mjini, Shilingi **3,479,681,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Magharibi "A" na Shilingi **4,275,441,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Magharibi "B".

**MKOA WA KASKAZINI UNGUJA (FUNGU 048)**

**128. Mheshimiwa Spika,** Fungu 048 (Mkoa wa Kaskazini Unguja) linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **6,645,467,000/=.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,087,742,000/=** ni mishahara, Shilingi **1,948,605,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **2,609,120,000/=** ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa Kaskazini 'A' na Baraza la Mji Kaskazini 'B'. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **25,700,000/=** yatakayokusanywa na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**129. Mheshimiwa Spika,** Ofisi inaomba kuidhinishiwa mapato ya shilingi **3,673,327,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Kaskazini "A" na Shilingi **1,957,114,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji Kaskazini "B".

**MKOA WA KUSINI UNGUJA (FUNGU O49)**

**130. Mheshimiwa Spika,** Fungu 049 (Mkoa wa Kusini Unguja) linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **6,372,776,000/=.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,173,170,000/=** ni mishahara, Shilingi **1,947,760,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **2,251,846,000/=** ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa Kati na Baraza la Mji Kusini. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **32,500,000/=** yatakayokusanywa na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

131. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi inaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **2,357,287,200/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Kati na Shilingi **2,175,287,200/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji Kusini.

**MKOA WA KUSINI PEMBA (FUNGU (050)**

132. **Mheshimiwa Spika,** Fungu 050 (Mkoa wa Kusini Pemba) linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **6,859,820,000/=.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,576,810,000/=** ni mishahara, Shilingi **1,358,760,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **3,924,250,000/=** ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **37,665,000/=** yatakayokusanywa na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

133. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi inaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **1,275,481,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Chake Chake na Shilingi **675,087,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mkoani.

**MKOA WA KASKAZINI PEMBA (FUNGU 051)**

134. **Mheshimiwa Spika,** Fungu 051 (Mkoa wa Kaskazini Pemba) linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi **6,432,390,000/=.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,841,430,000/=** ni mishahara, Shilingi **1,575,940,000/=** ni matumizi mengineyo na Shilingi **3,051,020,000/=** ni ruzuku kwa Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya Micheweni. Aidha, fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **7,500,000/=** yatakayokusanywa na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

135. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi inaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **525,758,000/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji Wete na Shilingi **625,582,000/=**

yatakayokusanywa na kutumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

## E. SHUKRANI

136. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mchango wake mkubwa na maendeleo ya Ofisi hii kwa lengo la kuongeza ufanisi juu ya upatikanaji wa huduma na kuwajengea wananchi miradi mbali mbali ya maendeleo.

137. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukrani kwa Washirika wa maendeleo ambao ni Benki ya Dunia, Umoja wa Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la (UNFPA), Shirika la Kuhudumia Watoto (UNICEF). Washirika hawa wametusaidia kifedha kutekeleza miradi yetu ya mazingira, ukuaji wa miji na hifadhi ya watoto.

138. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani maalum nazitoa kwa Katibu Mkuu Ndugu Issa Mahfoudh Haji, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mikidadi Mbarouk Mzee, Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wote, Mameya na Wenyeviti wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Masheha na watendaji wote.

139. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naishukuru familia yangu hususan Mke wangu na watoto wangu na familia kwa ujumla kwa uvumilivu wanaonionyesha wakati nikiendelea kutekeleza majukumu yangu ya kifamilia na kitaifa.

140. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kuwashukuru kwa dhati ya moyo wangu Baba yangu mzazi Bwana Kitwana Mustafa Makame na Mama yangu Bi Tatu Haji Makame, Baba na Mama zangu wakubwa na wadogo, Wajomba zangu, ndugu zangu na Jamaa zangu wote. Kwa hakika bila ya wao leo nisingeweza kusimama hapa.

142. **Mheshimiwa Spika,** Natoa shukrani zangu maalum kwa wananchi wenzangu wa Dunga, wananchi wenzangu wa Makunduchi na wananchi wenzangu wa Jimbo la Kwahani pamoja na marafiki zangu wote kwa kuendelea kuniombea dua na kunipa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

143. **Mheshimiwa Spika,** namalizia hotuba yangu kwa kuvishukuru vyombo vya habari kwa mchango wao katika kuhabarisha Wananchi juu ya matukio mbali mbali yanayohusu Wizara hii.

## F. HITIMISHO

144. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuweza kutekeleza malengo yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaiomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya Shilingi **695,735,989,000/=.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **217,830,612,000/=** kwa ajili ya mishahara, Shilingi **50,190,925,000/=** kwa matumizi mengineyo, Shilingi **20,518,426,000/=** ruzuku kwa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ, Wakala wa Ulinzi wa JKU na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shilingi **405,196,026,000/=** kwa matumizi ya kazi za maendeleo. **(Kiambatanisho nambari 10a, 10b na 11 kinafafanua zaidi)**

145. **Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Ofisi inaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi **8,817,956,000/=** kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali na kuidhinishiwa mapato ya ndani ya Shilingi **25,995,938,400/=** yatakayokusanywa na kutumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. **(Kiambatanisho nambari 12 na 13 kinafafanua zaidi)**

**146. Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

**MHE. IDRISSA KITWANA MUSTAFA**
**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ ZANZIBAR.**

## Kiambatanisho Namba 01: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA FEDHA KWA TAASISI ZA OR-TMSMIM KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

| FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026 | | | | | | MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026 (MIEZI 9) | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MSHAHARA | OC | RUZUKU | MSH&OC& RUZUKU | MAENDELEO | JUMLA | MSHAHARA | % | OC | % | RUZUKU | % | MSH&OC& RUZUKU | % | MAENDELEO | % | JUMLA | % |
| D01 | Afisi Kuu | 2,272,300,000 | 5,920,800,000.0 | 301,900,000 | **8,495,000,000** | 92,121,970,000 | **100,616,970,000** | 1,739,577,469 | 76.56 | 2,626,671,570 | 44.36 | 101,909,667 | 33.76 | **4,468,158,706.0** | 52.60 | 18,690,923,469 | 20.29 | **23,159,082,175** | **23.02** |
| D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 46,715,900,000 | 9,864,000,000.0 | 738,300,000 | **57,318,200,000** | 14,534,100,000 | **71,852,300,000** | 33,629,879,307 | 71.99 | 6,650,072,761 | 67.42 | 204,575,000 | 27.71 | **40,484,527,068.0** | 70.63 | 9,580,550,488 | 65.92 | **50,065,077,556** | 69.68 |
| D03 | Chuo cha mafunzo | 31,788,900,000 | 6,625,800,000.0 | - | **38,414,700,000** | 3,578,000,000 | **41,992,700,000** | 23,090,062,442 | 72.64 | 4,562,596,004 | 68.86 | - | 0.00 | **27,652,658,446.0** | 71.98 | 1,615,000,000 | 45.14 | **29,267,658,446** | 69.70 |
| D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 55,200,000,000 | 9,455,300,000.0 | - | **64,655,300,000** | 5,000,000,000 | **69,655,300,000** | 33,194,015,577 | 60.13 | 6,037,688,633 | 63.86 | - | 0.00 | **39,231,704,210.0** | 60.68 | 1,496,155,815 | 29.92 | **40,727,860,025** | 58.47 |
| D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 24,951,100,000 | 3,827,800,000.0 | - | **28,778,900,000** | 25,760,057,000 | **54,538,957,000** | 18,207,446,701 | 72.97 | 3,197,020,536 | 83.52 | - | 0.00 | **21,404,467,237.0** | 74.38 | 4,270,160,692 | 16.58 | **25,674,627,929** | 47.08 |
| D06 | Kikosi cha Valantia | 35,027,500,000 | 4,313,400,000.0 | - | **39,340,900,000** | 5,524,000,000 | **44,864,900,000** | 23,965,668,364 | 68.42 | 3,704,303,638 | 85.88 | - | 0.00 | **27,669,972,002.0** | 70.33 | 1,186,016,299 | 21.47 | **28,855,988,301** | 64.32 |
| **Jumla IM** | | **193,683,400,000** | **34,086,300,000.0** | **738,300,000** | **228,508,000,000** | **54,396,157,000** | **282,904,157,000** | **132,087,072,391** | 68.20 | **24,151,681,572** | 70.85 | **204,575,000** | 27.71 | **156,443,328,963.0** | **68.46** | **18,147,883,294** | **33.36** | **174,591,212,257** | 61.71 |
| D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 2,603,200,000 | 1,946,200,000.0 | 8,951,200,000 | **13,500,600,000** | 140,000,000 | **13,500,600,000** | 1,869,356,472.5 | 71.81 | 716,379,037 | 36.81 | 5,619,623,983 | 62.78 | **8,205,359,492.5** | 60.78 | - | 0.00 | **8,205,359,492.5** | 60.78 |
| D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 1,893,500,000 | 1,010,477,000.0 | 1,806,600,000 | **4,710,577,000** | 92,000,000 | **4,710,577,000** | 1,435,657,330 | 75.82 | 732,612,800 | 72.50 | 1,280,038,011 | 70.85 | **3,448,308,140.5** | 73.20 | 45,674,000 | 49.65 | **3,493,982,140.5** | 74.17 |
| D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 2,098,700,000 | 998,200,000.0 | 2,517,600,000 | **5,614,500,000** | 76,170,368.85 | **5,614,500,000** | 1,516,414,135 | 72.25 | 426,000,000 | 42.68 | 1,444,061,731.0 | 57.36 | **3,386,475,866.0** | 60.32 | 46,463,925 | 61.00 | **3,432,939,791.0** | 61.14 |
| D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 1,618,900,000 | 1,009,900,000.0 | 3,535,800,000 | **6,218,900,000** | 92,000,000 | **6,218,900,000** | 1,106,285,052.5 | 68.34 | 548,166,000 | 54.28 | 2,085,112,727.0 | 58.97 | **3,739,563,779.5** | 60.13 | 59,066,000 | 64.20 | **3,798,629,779.5** | 61.08 |
| D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 1,630,200,000 | 1,249,400,000.0 | 2,584,900,000 | **5,464,500,000** | 92,000,000 | **5,464,500,000** | 1,225,475,847.5 | 75.17 | 540,000,000 | 43.22 | 1,400,499,341 | 54.18 | **3,165,975,188.5** | 57.94 | 61,042,000 | 66.35 | **3,227,017,188.5** | 59.05 |
| **Jumla Mikoa** | | **9,844,500,000** | **6,214,177,000.0** | **19,396,100,000** | **35,509,077,000** | **492,170,368.85** | **35,509,077,000** | **7,153,188,838** | **72.66** | **2,963,157,837** | **47.68** | **11,829,335,793** | **60.99** | **21,945,682,467.0** | 61.80 | **212,245,925** | 43.12 | **22,157,928,392** | **62.40** |
| D12 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 3,185,700,000 | 2,248,500,000.0 | - | **5,434,200,000** | 3,500,000,000 | **8,934,200,000** | 2,235,413,826 | 70.17 | 997,409,178 | 44.36 | - | 0.00 | **3,232,823,004.0** | 59.49 | 1,347,251,067 | 38.49 | **4,580,074,071** | 51.26 |
| **Jumla Kuu** | | **208,985,900,000** | **48,469,777,000** | **20,436,300,000** | **277,946,277,000** | **150,018,127,000** | **427,910,104,000** | **143,215,252,524** | **68.53** | **30,738,920,157** | **63.42** | **12,135,820,460** | **59.38** | **186,089,993,140.0** | 66.95 | **38,398,303,755** | **25.60** | **224,488,296,895** | **52.46** |

**Kiambatanisho Namba 02: MAPATO YALIYOKUSANYWA NA KUPELEKWA HAZINA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI 2025/2026**

| FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2025/2026 | MAKUSANYO YA MIEZI TISA (9) | ASILIMIA ILIYOCHANGIWA |
|---|---|---|---|---|
| D01 | Afisi Kuu | 1,800,000,000 | 1,999,917,000 | 111 |
| D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 379,418,000 | 166,000,000 | 44 |
| | Wakala wa Ulinzi JKU | 2,700,000,000 | 504,869,342 | 19 |
| D03 | Chuo cha mafunzo | 297,089,000 | 180,700,000 | 61 |
| D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 290,760,000 | 50,000,000 | 17 |
| D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 458,138,000 | 132,061,000 | 29 |
| **Jumla Idara Maalum SMZ** | | **4,125,405,000** | **1,033,630,342** | **25** |
| D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 80,504,000 | 24,890,000 | 30.9 |
| D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 35,000,000 | 4,250,000 | 12.1 |
| D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 58,561,000 | 12,526,001 | 21.4 |
| D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 40,596,000 | 18,226,000 | 44.90 |
| D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 20,000,000 | 1,011,000 | 5 |
| **Jumla Mikoa** | | **234,661,000** | **60,903,001** | 26 |
| D12 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 4,698,004,000 | 1,254,861,650 | 27 |
| **JUMLA KUU** | | **10,858,070,000** | **4,349,311,993** | **40** |

**Kiambatanisho Namba 03: MAKUSANYO YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2025/2026**

| NO | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MIEZI TISA (9) | MAKUSANYO JULAI HADI MACHI 2025/2026 | ASILIMIA YA MAKUSANYO KWA MIEZI 9 | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BARAZA LA MANISPAA MJINI | 3,880,000,000 | 2,462,777,500 | 2,309,167,482 | 94 | 60 |
| 2 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A | 2,530,000,000 | 1,777,163,364 | 1,863,237,418 | 105 | 74 |
| 3 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 2,901,674,000 | 2,173,105,668 | 1,802,980,901 | 83 | 62 |
| 4 | BARAZA LA MANISPAA KATI | 1,955,000,000 | 1,355,000,000 | 1,061,107,761 | 78 | 54 |
| 5 | BARAZA LA MJI KUSINI | 1,243,740,000 | 696,890,535 | 1,156,198,670 | 166 | 93 |
| 6 | BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI A | 2,841,922,087 | 2,112,248,865 | 1,871,764,477 | 89 | 66 |
| 7 | BARAZA LA MJI KASKAZINI B | 1,534,500,000 | 1,193,829,000 | 878,797,852 | 74 | 57 |
| 8 | BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE | 880,788,000 | 660,772,650 | 621,795,075 | 94 | 71 |
| 9 | BARAZA LA MJI MKOANI | 426,640,000 | 311,647,187 | 464,932,437 | 149 | 109 |
| 10 | BARAZA LA MJI WETE | 505,000,000 | 376,733,001 | 325,710,925 | 86 | 64 |
| 11 | HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI | 470,000,000 | 340,000,000 | 339,553,312 | 100 | 72 |
| | **JUMLA** | **19,169,264,087.0** | **13,460,167,770** | **12,695,246,310** | **94** | **66** |

**Kiambatanisho Namba 04: OFISI ZA SHEHIA ZILIZOJENGWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

| S/No. | SHEHIA ZA UNGUJA | WILAYA |
|---|---|---|
| 1 | BUMBWISUDI | Magharibi A |
| 2 | MWAKAJE | |
| 3 | MICHIKICHINI | |
| 4 | MTOFAANI | |
| 5 | KISAUNI | Magharibi B |
| 6 | SOKONI | |
| 7 | MICHUNGWANI | |
| 8 | MATEMWE KASAKAZINI | Kaskazini A |
| 9 | MATEMWE MBUYU TENDE | |
| 10 | POTOA | |
| 11 | MOGA | |
| 12 | BANDAMAJI | |
| 13 | KIGUNDA | |
| 14 | DONGE NJIA YA MTONI | Kaskazini B |
| 15 | KIONGWE KIDOGO | |
| 16 | KITOPE | |
| 17 | MAHONDA | |
| 18 | MANGAPWANI | |
| 19 | KIONGONI | Kusini |
| 20 | DONGWE | |
| 21 | KITOGANI | |
| 22 | JAMBIANI KIBIGIJA | |
| 23 | BWEJUU | |
| 24 | BINGUNI | Kati |
| 25 | BUNGI | |
| 26 | JUMBI | |
| 27 | KOANI | |
| 28 | BAMBI | |
| 29 | MIWANI | |
| | **SHEHIA ZA PEMBA** | |
| 1 | FUNDO | Wete |
| 2 | KAMBINI | |
| 3 | MCHANGA MDOGO | |
| 4 | PEMBENI | |
| 5 | KOJANI | |
| 6 | FINYA | |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | KONDE | Micheweni |
| 8 | KINOE | |
| 9 | TUMBE MASHARIKI | |
| 10 | TUMBE MAGHARIBI | |
| 11 | KIUUYU MIBUYUNI | |
| 12 | SHANAKE | |
| 13 | MATALE | Chake Chake |
| 14 | MFIKIWA | |
| 15 | MCHANGAMRIMA | |
| 16 | MINAZINI | Mkoani |
| 17 | CHUMBAGENI | |
| 18 | KIWANI | |
| 19 | MIZINGANI | |
| **JUMLA SHEHIA UNGUJA NA PEMBA** | | **48** |

**Kiambatanisho Nambari 05: MAENEO YA UJENZI WA OFISI ZA WAHESHIMIWA WAKUU WA MIKOA**

| NO | MKOA | ENEO LA KUJENGWA OFISI |
|---|---|---|
| 1 | MKOA WA MJINI MAGHARIBI | MWANAKWEREKWE |
| 2 | MKOA WA KUSINI UNGUJA | TUNGUU |
| 3 | MKOA WA KASKAZINI UNGUJA | MKOKOTONI |
| 4 | MKOA WA KUSINI PEMBA | TIBIRINZI |
| 5 | MKOA WA KASKAZINI PEMBA | KINYASINI |

**Kiambatanisho Nambari 06: KUUNDWA KWA MABARAZA YA MADIWANI**

| No | BARAZA | MKOA |
|---|---|---|
| 1 | BARAZA LA JIJI ZANZIBAR | MKOA WA MJINI MAGHARIBI |
| 2 | BARAZA LA MANISPAA MJINI | |
| 3 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A | |
| 4 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | |
| 5 | BARAZA LA MANISPAA WILAYA YA KATI | MKOA WA KUSINI UNGUJA |
| 6 | BARAZA LA MJI KUSINI | |
| 7 | BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI A | MKOA WA KASKAZINI UNGUJA |
| 8 | BARAZA LA MJI KASKAZINI B | |
| 9 | BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE | MKOA WA KUSINI PEMBA |
| 10 | BARAZA LA MJI MKOANI | |
| 11 | BARAZA LA MJI WETE | MKOA WA KASKAZINI PEMBA |
| 12 | HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI | |

**Kiambatanisho Namba 07: USULUHISHI WA MIGOGORO YA ARDHI**

| TAASISI | IDADI YA MIGOGORO ILIYOPOKELEWA | MIGOGORO ILIYOTATULIWA | MIGOGORO INAYOENDELEA NA HATUA ZA UTATUZI |
|---|---|---|---|
| MKOA WA MJINI MAGHARIBI | 104 | 30 | 74 |
| MKOA WA KUSINI UNGUJA | 19 | 10 | 9 |
| MKOA WA KASKAZINI UNGUJA | 20 | 12 | 8 |
| MKOA WA KUSINI PEMBA | 14 | 4 | 10 |
| MKOA WA KASKAZINI PEMBA | 30 | 20 | 10 |
| **JUMLA** | **187** | **76** | **111** |

**Kiambatanisho Nambari 08: UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

| MKOA | IDADI YA MIRADI |
|---|---|
| MKOA WA MJINI MAGHARIBI | 47 |
| MKOA WA KUSINI UNGUJA | 18 |
| MKOA WA KASKAZINI UNGUJA | 17 |
| MKOA WA KUSINI PEMBA | 18 |
| MKOA WA KASKAZINI PEMBA | 16 |
| **JUMLA** | **116** |

**Kiambatanisho Nambari 09: MCHANGO WA FEDHA ZA UWEZESHAJI WA MAKUNDI MAALUM (4:4:2) 2025/2026**

| SN | TAASISI | FEDHA ZILIZOTOLEWA |
|---|---|---|
| 1 | BARAZA LA MANISPAA MJINI | 30,000,000.00 |
| 2 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A | 87,990,821.00 |
| 3 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 40,000,000.00 |
| 4 | BARAZA LA MANISPAA WILAYA YA KATI | 111,810,991.60 |
| 5 | BARAZA LA MJI KUSINI | 84,335,870.75 |
| 6 | BARAZA LA MJI KASKAZINI A | 58,202,654.30 |
| 7 | BARAZA LA MJI KASKAZINI B | 70,289,505.70 |
| 8 | BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE | 60,889,208.00 |
| 9 | BARAZA LA MJI MKOANI | 39,605,058.06 |
| 10 | BARAZA LA MJI WETE | 31,367,814.65 |
| 11 | HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI | 28,113,450.76 |
| | **JUMLA KUU** | **642,605,374.82** |

**Kiambatanisho Nambari 10a: Miradi Inayotarajiwa Kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027**

| NA. | WIZARA | SEKTA | GHARAMA | MUDA WA UTEKELEZAJI | MAHALI ULIPO MRADI | WANUFAIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Chuo cha Kijeshi cha Kisasa cha Idara Maalum za SMZ | Ulinzi na Usalama | 70,000,000,000 | Mwaka mmoja | Kikungwi | Maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ na vyombo vyengine vya Ulinzi na Usalama |
| 2 | Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ | Afya | 30,000,000,000 | Mwaka mmoja | Kama | Wananchi, Viongozi wa Serikali, Watalii, Maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ. |
| **Jumla ndogo** | | | **100,000,000,000** | | | |
| 3 | Mradi wa ujenzi wa Masoko ya Kibandamaiti na Kinyasini | Biashara na Masoko | 65,000,000,000 | Mwaka mmoja | Kibandamaiti, Kinyasini | Wananchi na Wajasiriamali wadogo |
| 4 | Mradi wa Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi katika Bwawa la Mwanakwerekwe | Usafiri wa Umma na Ukuaji wa Miji | 47,000,000,000 | Mwaka mmoja | Mwanakwerekwe | Wananchi |
| **Jumla ndogo** | | | **112,000,000,000** | | | |
| **Jumla kuu Miradi Mipya ya Kimkakati** | | | **212,000,000,000** | | | |

**Kiambatanisho Nambari 10b: Miradi Inayoendelea**

| B | MIRADI INAYOENDELEA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **JINA LA MRADI** | **SEKTA** | **GHARAMA** | **MUDA WA UTEKELEZAJI** | **MAHALI ULIPO MRADI** | **WANUFAIKA** |
| 5 | Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama | Ulinzi na Usalama | 40,175,619,000 | Mwaka mmoja | Unguja na Pemba | Wananchi na mali zao. |
| 6 | Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai (Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo cha Kisasa) | Mfumo wa Haki jinai (Sheria) | 40,000,000,000 | Mwaka mmoja | Hanyegwa Mchana | Wanafunzi na mahabusu wa Chuo cha Mafunzo |
| 7 | Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Shehia (Masheha) | Tawala za Mikoa | 40,000,000,000 | Mwaka mmoja | Shehia zote za Unguja na Pemba | Wananchi na Viongozi wa Shehia |
| 8 | Mradi wa usafi na upendezeshaji wa Miji | Serikali za Mitaa | 18,001,001,000 | Mwaka mmoja | Mkoa wa Mjini Magharibi | Wananchi |
| **Jumla ndogo** | | | **138,176,620,000** | | | |
| **Jumla Kuu Miradi inayoendelea** | | | **138,176,620,000** | | | |
| **Jumla Kuu Miradi yote** | | | **350,176,620,000** | | | |

**Kiambatanisho Nambari 11: MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

| IDARA | KAZI ZA KAWAIDA | | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MISHAHARA NA STAHIKI | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | JUMLA MISHAHARA&OC&RU | SMZ | WAHISANI | JUMLA MAENDELEO | |
| Afisi Kuu | 2,647,490,000 | 5,012,800,000 | 792,480,000 | **8,452,770,000** | 350,176,620,000 | 7,855,886,000 | **358,032,506,000** | **366,485,276,000** |
| Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 2,993,250,000 | 1,898,150,000 | - | **4,891,400,000** | 4,000,000,000 | 257,249,000 | **4,257,249,000** | **9,148,649,000.000** |
| Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) | 47,883,000,000 | 9,336,800,000 | 822,690,000 | **58,042,490,000** | 12,763,280,000 | - | **12,763,280,000** | **70,805,770,000** |
| Chuo cha mafunzo | 39,793,570,000 | 6,975,970,000 | - | **46,769,540,000** | 3,400,000,000 | | **3,400,000,000** | **50,169,540,000** |
| Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 51,200,000,000 | 8,346,280,000 | - | **59,546,280,000** | 12,784,000,000 | | **12,784,000,000** | **72,330,280,000** |
| Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 26,239,930,000 | 4,893,410,000 | - | **31,133,340,000** | 4,000,000,000 | 3,558,991,000 | **7,558,991,000** | **38,692,331,000** |
| Kikosi cha Valantia | 36,746,750,000 | 4,476,010,000 | - | **41,222,760,000** | 6,400,000,000 | - | **6,400,000,000** | **47,622,760,000** |
| Mkoa wa Mjini Magharibi | 2,647,470,000 | 2,420,440,000 | 9,103,020,000 | **14,170,930,000** | - | | **-** | **14,170,930,000** |
| Mkoa wa Kaksazini Unguja | 2,087,742,000 | 1,948,605,000 | 2,609,120,000 | **6,645,467,000** | - | - | **-** | **6,645,467,000** |
| Mkoa wa Kusini Unguja | 2,173,170,000 | 1,947,760,000 | 2,251,846,000 | **6,372,776,000** | - | | **-** | **6,372,776,000** |
| Mkoa wa Kusini Pemba | 1,576,810,000 | 1,358,760,000 | 3,924,250,000 | **6,859,820,000** | - | - | **-** | **6,859,820,000** |
| Mkoa wa Kaskazini Pemba | 1,841,430,000 | 1,575,940,000 | 3,015,020,000 | **6,432,390,000** | - | - | **-** | **6,432,390,000** |
| **JUMLA** | **217,830,612,000** | **50,190,925,000** | **22,518,426,000** | **290,539,963,000** | **393,523,900,000** | **11,672,126,000** | **405,196,026,000** | **695,735,989,000** |

**Kiambatanisho Nambari 12: MAKADIRIO YA MAKUSANYO YANAYOPELEKWA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

| FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO YA MAPATO 2026/2027 |
|---|---|---|---|
| 004 | Afisi Kuu | 1,800,000,000 | 1,875,000,000 |
| 041 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 4,698,004,000 | 3,253,999,000 |
| 042 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 379,418,000 | 675,000,000 |
| 043 | Wakala wa Ulinzi JKU | 2,700,000,000 | 1,650,000,000 |
| 044 | Chuo cha mafunzo | 297,089,000 | 375,000,000 |
| 045 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 290,760,000 | 375,700,000 |
| 046 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 458,138,000 | 467,500,000 |
| 047 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 80,504,000 | 42,392,000 |
| 048 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 35,000,000 | 25,700,000 |
| 049 | Mkoa wa Kusini Unguja | 58,561,000 | 32,500,000 |
| 050 | Mkoa wa Kusini Pemba | 40,596,000 | 37,665,000 |
| 051 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 20,000,000 | 7,500,000 |
| **JUMLA** | | **10,858,070,000** | **8,817,956,000.0** |

**Kiambatanisho Nambari 13: MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

| SN | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2025/2026 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2026/2027 | TOFAUTI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | BARAZA LA MANISPAA MJINI | 3,880,000,000 | 4,975,893,000 | 1,095,893,000 |
| 2 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A | 2,530,000,000 | 3,479,681,000 | 949,681,000 |
| 3 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 2,901,674,000 | 4,275,441,000 | 1,373,767,000 |
| 4 | BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI A | 2,841,922,087 | 3,673,327,000 | 831,404,913 |
| 5 | BARAZA LA MJI KASKAZINI B | 1,534,500,000 | 1,957,114,000 | 422,614,000 |
| 6 | BARAZA LA MANISPAA KATI | 1,955,000,000 | 2,357,287,200 | 402,287,200 |
| 7 | BARAZA LA MJI KUSINI | 1,243,740,000 | 2,175,287,200 | 931,547,200 |
| 8 | BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE | 880,788,000 | 1,275,481,000 | 394,693,000 |
| 9 | BARAZA LA MJI MKOANI | 426,640,000 | 675,087,000 | 248,447,000 |
| 10 | BARAZA LA MJI WETE | 505,000,000 | 525,758,000 | 20,758,000 |
| 11 | HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI | 470,000,000 | 625,582,000 | 155,582,000 |
| | **JUMLA KUU** | **19,169,264,087** | **25,995,938,400** | **6,826,674,313** |